**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

**IDARA YA MISITU NA NYUKI**

# TANGAZO LA KUITISHA MAANDIKO YA KUOMBA FEDHA ZA TOZO YA UPANDAJI MITI KWA AJILI YA KUGHARAMIA SHUGHULI ZA UPANDAJI MITI NA KUBORESHA UHIFADHI WA MISITU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**SEPTEMBA, 2026**

## 1. UTANGULIZI

Wizara ya Maliasili na Utalii iliandaa "Mwongozo wa Uvunaji Endelevu na Biashara ya Mazao ya Misitu yanayovunwa katika Misitu ya Asili" wa mwaka 2017 ambao umeweka utaratibu kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu kutoka misitu ya asili kulipa tozo ya upandaji miti inayojulikana kwa lugha ya Kiingereza kama *"5% tree planting levy"*. Aidha, fedha zitokanazo na tozo ya upandaji miti zinapaswa kutumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za upandaji miti na kuboresha uhifadhi wa misitu. Lengo la tozo hiyo ni kuchangia urejeshaji wa uoto wa asili na kuongoa maeneo yaliyoharibika kupitia upandaji miti na njia nyingine za kuboresha uhifadhi wa misitu. Vilevile, kwa mujibu wa miongozo iliyopo, fedha za tozo ya upandaji miti zinakusanywa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na kuwasilishwa Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF). Aidha, Mfuko una jukumu la kutoa fedha hizo kwa wadau husika ili zitumike kuchangia urejeshaji wa uoto wa asili na kuongoa maeneo yaliyoharibika kupitia upandaji miti na njia nyingine za kuboresha uhifadhi wa misitu.

Katika kufanikisha utekelezaji Mwongozo wa uvunaji endelevu na biashara ya mazao ya misitu yanayovunwa katika misitu ya asili, Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) na iliyokuwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (kwa sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - OWM, TAMISEMI), zilisasaini Hati ya Makubaliano (*Memorandum of Understanding* - MoU). Lengo la MoU hiyo ni kuboresha ukusanyaji, utoaji, matumizi, usimamizi na ufuatiliaji wa fedha za tozo ya upandaji miti. Aidha, kupitia MoU hiyo, Kamati ya kuratibu utekelezaji wa MoU na kusimamia tozo ya upandaji miti imeanzishwa. Kamati ina Wajumbe watano (5) kutoka MNRT, OWM - TAMISEMI, TFS, TaFF na mwakilishi wa wafanyabiashara wa mazao ya misitu yanayovunwa katika misitu ya asili.

Ufuatiliji na tathmini ya matumizi ya fedha za tozo ya upandaji miti ulibaini kuwa utaratibu uliokuwa unatumika hapo awali wa kutoa fedha za tozo ya upandaji miti kwa halmashauri ya wilaya ilipokusanywa tozo hiyo ulikuwa wa kibaguzi na baadhi ya halmashauri hazikujipanga kupokea fedha hizo na hivyo kusababisha fedha za tozo ya upandaji miti kutumika kutekeleza shughuli nyingine ambazo hazihusiani na upandaji miti na uhifadhi wa misitu. Aidha, utaratibu ulisababisha changamoto ya kukosekana kwa vifungu vya kulipia fedha za tozo ya upandaji miti katika mpango na bajeti za halmashauri na hivyo kutoingizwa zinazotekelezwa kwa kutumia tozo hiyo katika bajeti za mwaka husika. Kutokana na changamoto hizo, likajitokeza hitaji la kuandaa utaratibu mzuri wa ukusanyaji, utoaji, matumizi, usimamizi na ufuatiliaji wa fedha za tozo ya upandaji miti.

Kufuatia kubainika kwa changamoto kwenye utaratibu uliokuwa ikitumika wa kutoa fedha za tozo ya upandaji miti, mwaka 2022 ulitolewa **Mwongozo** ulioweka utaratibu mzuri wa ukusanyaji, utoaji, matumizi, usimamizi na ufuatiliaji wa fedha za tozo ya upandaji miti. Kwa mujibu wa mwongozo huo, fedha za tozo ya upandaji miti zinatolewa baada ya kuwasilishwa kwa maandiko ya kuomba fedha hizo na maandiko hayo kukidhi vigezo na kuidhinishwa kwa ajili ya kupatiwa fedha za tozo ya upandaji miti. Hivyo, kupitia tangazo hili walengwa wanahimizwa kuwasilisha maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti kwa kuzingatia vigezo vilivyopo.

## 2. WALENGWA (WANAOWEZA KUOMBA RUZUKU) YA FEDHA ZITOKANAZO NA TOZO YA UPANDAJI MITI

Walengwa wa fedha za tozo ya upandaji miti ni Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji na TFS. Aidha, halmshauri inaweza kuandaa andiko la kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa ajili ya kupanda miti kwenye ardhi inayomilikiwa na wadau wengine kama shule na magereza. Iwapo halmshauri itawasilisha andiko la kupanda miti kwenye ardhi inayomilikiwa na wadau wengine kama shule na magereza, andiko hilo linapaswa kuambatishwa mkataba wa makubaliano ya kupanda miti katika ardhi ya shule na magereza husika, na mkataba unapaswa kuandaliwa kisheria na kusainiwa kati ya halmashauri husika na shule na magereza husika. Sambamba na hilo, vigezo na masharti vilivyooneshwa katika kipengele namba 2.1 vinapaswa kuzingatiwa ipasavyo wakati wa kuomba fedha za tozo ya upandaji miti.

### 2.1 Vigezo na Masharti ya Kuzingatiwa wakati wa Kuomba Fedha za Tozo ya Upandaji Miti

Vigezo na masharti yaliyoainishwa katika kipengele namba (i) hadi kipengele namba (ix) vinapaswa kuzingatiwa ipasavyo wakati wa kuomba fedha za tozo ya upandaji miti:

i) Kuwepo kwa andiko la kuomba fedha za tozo ya upandaji miti lililoandaliwa kwa kuzingatia muundo uliooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 1** cha tangazo hili;

ii) Kuwepo kwa eneo au maeneo ya kupanda miti yenye ukubwa **usiopungua hekta 30,** pamoja na kuwepo kwa mpango au mkakati wa kupanda na kutunza miti itakayopandwa na mpango au mkakati kuendeleza eneo au maeneo yatakayopandwa miti;

iii) Andiko lioneshe idadi ya miche ya miti itakayozalishwa, umiliki wa eneo au maeneo yatakayopandwa miti (kuwepo na taarifa zinazoonesha nani anamiliki eneo au maeneo yatakayopandwa miti), na ukubwa wa maeneo yatakayopandwa miti;

iv) Kuwepo kwa mpango au mkakati wa kurejesha uoto katika misitu ya hifadhi iliyoharibika (kwa miradi ya urejeshaji wa uoto wa asili au uoto uliopotea katika misitu ya hifadhi). Aidha, maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi inayohusiana na urejeshaji wa uoto wa asili au uoto uliopotea yanaweza kujumuisha ununuzi wa vyombo vya usafiri kama pikipiki au gari, na/au ujenzi wa vituo vya waangalizi wa misitu (*ranger posts*) ili kuimarisha ulinzi na kuzuia uharibifu wa misitu ya hifadhi;

v) Andiko liwe na taarifa zinazojitosheleza za kushawishi kupatiwa fedha za tozo ya upandaji miti kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri kama pikipiki au gari, na/au ujenzi wa vituo vya waangalizi wa misitu (*ranger posts*);

vi) Kuwepo kwa uthibitisho wa namna jamii inayozunguka maeneo mradi utakapotekelezwa itakavyoshirikishwa katika utekelezaji wa mradi;

vii) Andiko lioneshe kuwa matokeo ya utekelezaji wa mradi unaoombewa fedha za tozo ya upandaji miti yatachangia kuboresha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu, na kuchangia uendelezaji wa rasilimali misitu;

viii) Kuwepo kwa mpango wa kuufanya mradi unaoombewa fedha za tozo ya upandaji miti kuwa endelevu kwa kuonesha namna mradi utakavyoendelea kutekelezwa baada ya ukomo wa ruzuku ya fedha za tozo ya upandaji miti;

ix) Katika andiko la maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti kwa ajili ya miradi ya upandaji miti, mpango kazi na bajeti vioneshe kuwa zaidi ya asilimia 70 (70%) ya fedha za tozo ya upandaji miti itatumika kutekeleza shughuli mahususi za upandaji miti (ununuzi wa vifaa na mbegu, na mahitaji mengine ya kuwezesha uanzishwaji wa vitalu vya miti; uandaaji wa mashamba, upandaji miti na kuandaa mpango au mkakati wa usimamizi wa miti itakayopandwa, na kuendeleza eneo au maeneo yatakayopandwa miti); na

x) Katika andiko la maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri kama pikipiki au gari, na/au ujenzi wa vituo vya waangalizi wa misitu (*ranger posts*) mpango kazi na bajeti vioneshe kuwa fedha zote zitatumika kugharamia ununuzi wa vyombo vya usafiri au ujenzi wa *ranger posts*; na

xi) Kwa miradi yote inayohusika na ujenzi wa *ranger posts* waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti wanapaswa kuwasilisha ramani, michoro na mchanganuo wa gharama (BoQ). Aidha, kwa miradi ya ununuzi wa vyombo vya usafiri waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti wawasilishe vidadisi bei (*quotation*) vinavyoonesha gharama halisi ya chombo husika cha usafiri.

## 3. UTARATIBU WA KUOMBA NA KIASI CHA FEDHA KINACHOWEZA KUOMBWA

Kila mlengwa wa fedha za tozo ya upandaji miti atawasilishwa andiko moja la kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa kuzingatia yafuatayo:

3.1 Kiasi cha fedha kitakachoombwa kwa andiko moja la mradi wa upandaji miti kitategemea ukubwa eneo au maeneo yatakayopandwa miti kwa uwiano wa **shilingi 1,000,000/=** kwa hekta moja. Hivyo, waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti wanapaswa kuhakikisha kuwa, kiasi cha fedha kinachoombwa kinaendana/kinaoana na ukubwa wa eneo au maeneo yatakayopandwa miti.

3.2 Kwa walengwa wa fedha za tozo ya upandaji miti wanaotarajia kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri na ujenzi wa vituo vya waangalizi wa misitu (*ranger posts*), kiasi cha fedha kinapaswa kulingana na kiasi cha fedha kilichopo kwenye mchanganuo wa gharama (BoQ) au kiasi cha fedha kilichopo kwenye vidadisi bei (*quotation*).

## 4. KUANDAA NA KUWASILISHA MAOMBI YA FEDHA ZA TOZO YA UPANDAJI MITI

### 4.1 Kuandaa Maandiko kwa ajili ya Kuomba Fedha za Tozo ya Upandaji Miti

Maandiko kwa ajili ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti yanapaswa kutayarishwa/kuandaliwa kwa kufuata muundo uliooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 1** cha tangazo hili. Maandiko kwa ajili ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti yasizidi kurasa 15 ukiondoa viambatisho. Aidha, viambatisho vifuatavyo vinapaswa kuwasilishwa wakati wa kuwasilisha maandiko ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti:

i) Uthibitisho wa uwepo, umiliki na ukubwa wa eneo au maeneo yatakayopandwa miti;

ii) Barua *(covering letter)* ya kuwasilisha maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti iliyosainiwa na Mkurugenzi wa halmashauri husika au Kamishana wa Uhifadhi wa TFS;

iii) Bao la Mantiki *(Log Frame ya mradi)* linaloonesha malengo/madhumuni ya mradi, viashiria vya utendaji *(performance indicators),* matokeo yatarajiwayo kutoka kwenye mradi na shughuli zitakazotekelezwa; na

iv) Kwa walengwa wa fedha za tozo ya upandaji miti wanaotarajia kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri na ujenzi wa vituo vya waangalizi wa misitu (*ranger posts*), kiasi cha fedha kinapaswa kulingana na kiasi cha fedha kilichopo kwenye mchanganuo wa gharama (BoQ) au kiasi cha fedha kilichopo kwenye vidadisi bei (*quotation*).

***ANGALIZO: Maandiko ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti ambayo yatafanana au yatakuwa na vipengele vinavyofanana hayatapatiwa fedha kwa kuwa ni vigumu kutofautisha andiko lililoandaliwa na andiko lililonakiliwa kutoka maandiko mengine.***

4.2 **Kuwasilisha Maandiko kwa ajili ya Kuomba Fedha za Tozo ya Upandaji Miti**

Waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti wanahimizwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya kielektroniki *(online application)* ambapo wataingia katika mfumo kwa kutumia anuani *(link)* ifuatayo: **https://portal.maliasili.go.tz/** Baada ya kuingia kwenye mfumo, waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti watajisajili na kufuata maelekezo ya kuwawezesha kuweka taarifa zao, na kuweka *(upload)* andiko la kuomba fedha za tozo ya upandaji miti (likiwa katika PDF) na viambatisho husika na kuwasilisha. Atakayepata tatizo wakati wa kujisajili au wakati wa kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa kutumia mfumo wa kielektroniki, anaweza kuwasiliana na Mtaalam wa TEHAMA kupitia namba za simu **0714 580 688** kwa ajili ya kupata msaada.

Kwa kurahisisha uwasilishwaji wa maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti, unaweza kufuata hatua zifuatazo:

i) Kabla ya kuingia kwenye mfumo, waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti watapaswa kuandaa andiko la kuomba fedha kwa kufuata muundo uliooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 1;

ii) Kuweka maandiko ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwenye muundo wa **PDF**;

iii) Kuandaa viambatisho vyote muhimu na kuviweka kwenye muundo wa **PDF**; na

iv) Baada ya kukamilisha maandilizi na andiko na viambatisho vyote muhimu, waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti wataingia kwenye mfumo na kujisajili, kisha kuweka *(upload)* andiko na viambatisho husika na kuwasilisha.

Waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti watakaowasilisha maombi yao kwa kutumia mfumo wa kielektroniki watapokea ujumbe mfupi wa maneno kwenye simu za mkononi kuwajulisha kuhusu kupokelewa kwa maombi yao. Hivyo, waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti wanashauriwa kuandika namba za simu za mkononi za atakayekuwa mratibu wa mradi katika sehemu iliyoandikwa **Jina na Anwani ya Mratibu wa Mradi** kwenye muundo wa kuandaa maandiko kwa ajili ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti. Aidha, kwa waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti watakaoshindwa kabisa kuwasilisha maandiko ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa njia ya kielektroniki *(online application)*, wanaweza kuwasilisha maombi yao kwa njia ya posta kupitia anwani ifuatayo:

Mtendaji Mkuu,
Mfuko wa Misitu Tanzania,
Jengo la Bodi ya Mfuko wa Barabara,
S.L.P. 1764,
**DODOMA.**

Vilevile, waombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti wanaweza kuwasilisha maombi yao moja kwa moja katika Ofisi ya Mfuko wa Msitu Tanzania. Inasisitizwa kuwa atakayewasilisha maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti moja kwa moja katika Ofisi ya Mfuko wa Msitu Tanzania awe na *"dispatch"* na ahakikishe kuwa imesainiwa na atakayepokea maombi hayo.

Maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti yatakayowasilishwa kwa njia ya posta yataingizwa kwenye mfumo wa kielektroniki na waombaji wa ruzuku watapokea ujumbe kwenye simu zao za mkononi kuwajulisha kuhusu kupokelewa kwa maandiko ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti. Hivyo, waombaji wanahimizwa kuandika namba za simu za mkononi za atakayekuwa mratibu wakati wa utekelezaji katika sehemu iliyoandikwa **Jina na Anwani ya Mratibu wa Mradi** kwenye muundo wa kuandaa maandiko kwa ajili ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti.

***ANGALIZO: Maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti yatakayowasilishwa kwa njia ya baruapepe hayatashughulikiwa kwa kuwa waombaji wenye uwezo wa kutumia baruapepe wanashauriwa kutumia mfumo wa kielekroniki kuwasilisha maombi yao.***

***Mwisho wa kuwasilisha maandiko kwa ajili ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti ni tarehe 30 Oktoba, 2026.*** **Aidha,** ***Maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti yatakayowasilishwa baada ya tarehe 30 Oktoba, 2026 hayatashughulikiwa.***

## 5. UCHAMBUZI NA UHAKIKI WA MAOMBI, NA UAMUZI WA KUTOA FEDHA ZA TOZO YA UPANDAJI MITI

Maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti yatakayoopokelwa yatafanyiwa uchambuzi wa uchambuzi na uhakiki kwa kuzingatia mwongozo wa utoaji fedha hizo. Aidha, uamuzi wa kupatiwa au kutopatiwa fedha za tozo ya upandaji miti utatolewa kwa kuzingatia Kanuni za misitu za utoaji ruzuku zinazojulikana kwa lugha ya kiingereza kama ***"The Forest*** **(*Manner and Criteria for Awarding Grants*)** ***Regulations, 2021" (GN 266)***. Baada ya uamuzi kutolewa malipo ya fedha za tozo ya upandaji miti yatafanyika kwa waombaji waliodhinishwa kupatiwa fedha hizo.

**TANGAZO HILI LIMEANDALIWA NA KAMATI YA KUSIMAMIA FEDHA ZA TOZO YA UPANDAJI MITI NA LIMETOLEWA NA IDARA YA MISITU NA NYUKI KUPITIA KAMATI YA KUSIMAMIA FEDHA ZA TOZO YA UPANDAJI MITI**

**MWENYEKITI WA KAMATI:**

**JINA:** SELEBONI J. MUSHI

**SAINI**............................................

**TAREHE** 15.09.2026

## KIAMBATISHO NA. 1: MUUNDO WA KUANDAA ANDIKO KWA AJILI YA KUOMBA FEDHA ZA ZA TOZO YA UPANDAJI MITI

### 1. UTANGULIZI

i) Tafadhali andaa andiko la kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa kufuata muundo na maelekezo yaliyotolewa.

ii) Maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti yawe nadhifu, mepesi kusomeka na yawe na fonti ya *Arial*, pointi 12 na nafasi kati ya sentensi iwe 1.5.

### 2. TAARIFA ZA MSINGI KUHUSU ANDIKO LA MRADI

2.1 **Jina la Mradi *(Project Title):***

Jina la mradi liwe fupi, linaloeleweka na linalojitosheleza.

..........................................................................................................

..........................................................................................................

2.2 **Jina na Anwani ya Mwombaji**:

Kinachopaswa kuandikwa hapa ni jina la Taasisi (kwa kirefu na kifupisho kama kipo), na kwenye anwani ya mwombaji yanayopaswa kuandikwa ni wadhifa au cheo cha Mkuu wa Taasisi, halafu kuweka anwani ya posta, namba za simu za ofisi, nukushi na anwani ya barua pepe ya Taasisi yako.

..........................................................................................................

..........................................................................................................

2.3 **Jina na Anwani ya Mratibu wa Mradi:**

Kinachopaswa kuandikwa hapa ni jina la Mratibu wa Mradi ambaye ni mtumishi atakayeteuliwa na Mkuu wa Taasisi. Mwombaji anapaswa kuandika pia anwani ya posta, namba za simu ya mkononi ya Mratibu wa Mradi na anwani ya barua pepe ya Mratibu wa Mradi.

..........................................................................................................

..........................................................................................................

2.4 **Mahali Mradi utakapotekelezwa:**

Kinachopaswa kuandikwa kwenye kipengele hiki ni kutaja kijiji, kata, wilaya na mikoa mradi utakapotekelezwa.

..........................................................................................................

..........................................................................................................

2.5 **Aina ya Ruzuku:**

Mwombaji anapaswa kuandika kuwa anaomba ruzuku ya fedha za tozo ya upandaji miti.

..........................................................................................................

2.6 **Aina ya Uwezeshwaji:**

Mwombaji anapaswa kuandika kuwa anaomba fedha za tozo ya upandaji miti.

..........................................................................................................................

2.7 **Jumla ya Gharama za Mradi (Shilingi):**

Kinachopaswa kuandikwa hapa ni gharama zote za mradi zikijumuisha fedha zitakazotolewa fedha za tozo ya upandaji miti zinazoombwa kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania, na mchango wa mwombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti na michango ya wadau wengine kama wapo.

..........................................................................................................................

2.8 **Kiasi cha Fedha za Tozo za Upandaji Miti Kinachoombwa** kutoka Mfuko wa Misitu Tanzania **(Shilingi):**

..........................................................................................................................

2.9 **Mchango wa Mwombaji wa Fedha za Tozo ya Upandaji Miti na Michango Mingine:**

Kinachopaswa kuandikwa hapa ni kiasi cha fedha kitakachotolewa kama mchango Taasisi inayoomba fedha za tozo ya upandaji miti na michango ya wadau wengine kama wapo.

..........................................................................................................................

2.10 Muda wa utekelezaji wa mradi na mwezi ambao utekelezaji utaanza:

..........................................................................................................................

3. **Utangulizi (Usuli wa Mradi):**

Kinachopaswa kuandikwa hapa ni maelezo kwa kifupi kuhusu Taasisi inayoomba fedha za tozo ya upandaji miti, taarifa kwa kifupi kuhusu mradi unaoombewa fedha za tozo ya upandaji miti (taarifa ioneshe iwapo shughuli zinazoombewa fedha za tozo ya upandaji miti zilishaanza kutekelezwa au utekelezaji wake utaanza baada ya kupatiwa fedha hizo). Sehemu hii ni muhimu ili kujua kama kuna muendelezo wa shughuli au shughuli zitaanza kutekelezwa baada ya kupatiwa fedha za tozo ya upandaji miti. Ni muhimu pia kuweka taarifa kuhusu uwepo, umiliki na ukubwa wa eneo au maaeneo yatakayopandwa miti, taarifa kuhusu mkataba wa wadau watakaopatiwa miche ya miti na maeneo watakakopanda. Aidha, ni muhimu kuweka taarifa kuhusu jina, aina, umiliki na ukubwa wa msitu au misitu ya hifadhi inayoombewa fedha za tozo ya upandaji miti kwa ajili ya kuboresha uhifadhi wa msitunau misitu hiyo kupitia ununuzi wa vyombo vya usafiri na ujenzi wa vituo vya waangalizi wa misitu (*ranger posts*).

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

4. **Mantiki na Uthibitisho wa Mradi *(Rationale and Justification):***

Kinachopaswa kuandikwa katika kipengele hiki ni changamoto au tatizo lililowasukuma kuomba fedha za tozo ya upandaji miti na jinsi upatikanaji wa fedha hizo utakavyochangia utatuzi wa changamoto au tatizo hilo. Aidha, mnapaswa kuonesha jitihada ambazo zilikwishafanywa au zinazoendelea kufanywa katika kushughulikia changamoto au kutatua tatizo hilo. Mwombaji anapaswa kuonesha pia jinsi utekelezaji wa mradi utakavyochangia uendelezaji wa misitu au kuboresha uhifadhi na usimamizi wa rasilimali misitu katika eneo la utekelezaji wa mradi na Taifa kwa ujumla.

....................................................................................................................................

5. **Malengo ya Mradi na Viashiria vya Utendaji (*Performance Indicators*):**

Kinachopaswa kuandikwa katika kipengele hiki ni lengo kuu la mradi *(overall project objective),* ambalo litaandikwa kutokana na jina la mradi, malengo mahususi ya mradi *(specific project objectives)* na kila lengo mahususi lioanishwe na viashiria vyake vya utendaji. Mwombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti anashauriwa kutumia jedwali kuoanisha malengo mahususi ya mradi na viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa hapa chini.

| **Lengo mahususi la mradi** | **Viashiria vya utendaji** |
|---|---|
| **Lengo Na.1:** | 1. |
| | 2 |
| **Lengo Na.2:** | 1. |
| | 2. |
| **Lengo Na.3:** | 1. |
| | 2. |

6. **Matokeo Yanayotarajiwa kutoka kwenye Mradi:**

Kinachopaswa kuandikwa katika kipengele hiki ni yanayotarajiwa kuonekana baada ya kutekeleza shughuli za mradi. Sehemu hii ni muhimu kwa kuwa itasaidia ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za mradi unaoombewa fedha za tozo ya upandaji miti.

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

7. **Shughuli za Mradi Zitakazotekelezwa ili kufikia Matokeo:**

Kinachopaswa kuandikwa katika kipengele hiki ni shughuli zote za mradi zitakazotekelezwa ili kufikia matokeo tarajiwa ya mradi unaoombewa fedha za tozo ya upandaji miti.

....................................................................................................................................

....................................................................................................................................

8. **Mpango Kazi au Ratiba ya utekelezaji wa Mradi:**

Mwombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti anapaswa kuweka ratiba ya utekelezaji wa shughuli zote zitakazoainishwa katika kipengele namba 7 hapo juu.

..........................................................................................................................

9. **Mbinu za Kutekeleza Mradi:**

Katika sehemu hii mwombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti anatakiwa kuweka bayana jinsi shughuli za mradi zitakavyotekelezwa ili kufikia matokeo yanayokusudiwa. Shughuli za mradi zitakazotekelezwa ziainishwe na mbinu za utekelezaji wa kila shughuli zioneshwe. Aidha, michango ya wadau wengine katika kufanikisha utekelezaji wa mradi iwekwe bayana.

..........................................................................................................................

10. **Vichocheo vya Mafanikio**

Mwombaji wa ruzuku aeleze na kuchambua vichocheo ambavyo vina athari chanya katika kufikia mafanikio ya mradi na vichocheo ambavyo vina athari hasi kufikia mafanikio ya mradi. Aidha, mwombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti aeleze jinsi ya kukabiliana na vichocheo ambavyo vina athari hasi kufikia mafanikio ya mradi. Uchambuzi wa vichocheo hivyo unatakiwa utilie maanani muktadha wa mradi mzima na uwezo na ueledi wa watakaohusika na utekelezaji wa mradi.

..........................................................................................................................

11. **Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini**

Sehemu hii inapaswa kueleza namna mradi utakavyofanyiwa ufuatiliaji na tathmini katika kipindi chote cha utekelezaji wake. Kuwepo na maelezo ya vigezo vitakavyotumika kupima iwapo utekelezaji wa shughuli za mradi utaleta mabadiliko kwenye tatizo au utachangia utatuzi wa changamoto ambazo mradi umelenga kuzitatua. Aidha, mwombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti anapaswa kutoa ufafanuzi wa namna ya kupima mafanikio ya mradi. Ni muhimu pia kutambua kuwa bao la mantiki linaloonesha malengo ya mradi, shughuli na matokeo tarajiwa ya mradi linapaswa kutayarishwa ili kusaidia ufuatiliaji wa maendeleo ya mradi.

..........................................................................................................................

12. **Mpango wa Uendelevu wa Mradi**

Sehemu hii inapaswa kuelezea namna mradi unaoombewa fedha za tozo ya upandaji miti utakavyoendelea kutekelezwa baada ya ukomo wa ruzuku ya fedha za tozo ya upandaji miti. Sehemu hii ni muhimu kwa kuwa itatoa picha halisi ya mchango wa mradi katika kuboresha uhifadhi na usimamizi wa misitu. Aidha, ni vizuri ikafahamika kuwa maandiko ya miradi ambayo hayatakuwa na mpango wa uendelevu wa mradi, hayatafikiriwa kupatiwa fedha za tozo ya upandaji miti.

......................................................................................................

......................................................................................................

**13. Faida za Utekelezaji wa Mradi kwa Taifa**

Sehemu hii inapaswa kuelezea namna utekelezaji wa mradi utakavyofaidisha Taifa la Tanzania, na kueleza kwa nini kwa mradi wako upatiwe fedha za tozo ya upandaji miti. Hii ni sehemu muhimu ambayo inapaswa kuonesha matokeo fuasi ya mradi *(project outcomes).*

......................................................................................................

......................................................................................................

**14. Bajeti ya Mradi Unaoombewa Fedha za Tozo ya Upandaji Miti**

Mwombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti anapaswa kuandaa bajeti ya mradi kwa kufuata maelekezo yaliyopo kwenye Jedwali hapo chini. Bajeti ya fedha za tozo ya upandaji miti inapaswa kuwa na maelezo yanayoonesha namna kila kiasi kilivyokokotolewa na uhitaji na matumizi kwa kila shughuli na kipengele. Vipengele vifuatavyo visioneshwe kwenye bajeti kwani havitagharimiwa na fedha za tozo ya upandaji miti: mishahara ya watumishi, gharama za vifaa vya ofisi ya mwombaji, malipo saa za ziada *(extra duty allowance),* tuzo na gharama nyingine ambazo hazihusiani moja kwa moja na mradi unaoombewa fedha za tozo ya upandaji miti.

| **Shughuli and vipengele** | **Kipimo (Kizio)** | **Kiasi** | **Gharama ya Kizio (TZS)** | **Jumla ya Gharama (TZS)** |
|---|---|---|---|---|
| Shughuli zitakazotekelezwa | | | | |
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| **Jumla ya gharama ya mradi (Shilingi)** | | | | |
| **Kiasi cha fedha za tozo ya upandaji miti kinachoombwa (Shilingi)** | | | | |
| **Mchango wa mwombaji wa fedha za tozo ya upandaji miti (Shilingi)** | | | | |
| **Mchango kutoka kwa wadau wengine (Shilingi)** | | | | |

**15. RIDHAA:**

**15.1 Maoni na Mapendekezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri au Kamishna wa Uhifadhi wa TFS:**

Maoni na Mapendekezo:------------------------------------------------------------

Jina la Taasisi:------------------------------------------------------------

Jina la Kiongozi Mkuu wa Taasisi:------------------------------------------------------------

Cheo:------------------------------------------------------------

Saini:----------------------------------------------Tarehe:------------------------------------------

Mhuri rasmi:------------------------------------------------------------

## 16. VIAMBATISHO

Viambatisho vifuatavyo vinapaswa kuwasilishwa wakati wa kuwasilisha andiko la kuomba fedha za tozo ya upandaji miti:

16.1 Barua *(covering letter)* ya kuwasilisha maombi ya fedha za tozo ya upandaji miti iliyosainiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri husika au Kamishana wa Uhifadhi wa TFS;

16.2 Bao la Mantiki *(Log Frame ya mradi)* linaloonesha malengo/madhumuni ya mradi, viashiria vya utendaji *(performance indicators),* matokeo yatarajiwayo kutoka kwenye mradi na shughuli zitakazotekelezwa;

16.3 Uthibitisho wa uwepo, umiliki na ukubwa wa eneo au maeneo yatakayopandwa miti yasipongua hekta 30; na

16.4 Endapo halmshauri itawasilisha andiko la kupanda miti kwenye ardhi inayomilikiwa na wadau wengine kama shule na magereza, mkataba wa makubaliano ya kupanda miti katika ardhi ya shule na magereza husika, na mkataba huo unapaswa kuandaliwa kisheria na kusainiwa kati ya halmashauri husika na shule na magereza husika; na

16.5 Kwa walengwa wa fedha za tozo ya upandaji miti wanaotarajia kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri na ujenzi wa vituo vya waangalizi wa misitu (*ranger posts*), kiasi cha fedha kinapaswa kulingana na kiasi cha fedha kilichopo kwenye mchanganuo wa gharama (BoQ) au kiasi cha fedha kilichopo kwenye vidadisi bei (*quotation*).

---